JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**
**SHAURI NA. 04 - 2019/2020**

# GLOBAL TV

# UAMUZI

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa huduma za utangazaji kwa Global TV, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yoyote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Mnamo tarehe 10 Agosti, 2019, Global TV kupitia chaneli yake walirusha na kuonyesha miili ya watu waliofariki dunia katika ajali ya gari la mafuta ambalo lilianguka na kuwaka moto eneo la Msamvu mkoani Morogoro. Mtangazaji wa Global TV, Bwana Lucas Masungwa alitoa taarifa kuhusu ajali hiyo na hali picha ya miili ya watu walioungua vibaya ikionyeshwa na kuonekana kwa uwazi na watazamaji kinyume na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018 na maadili ya uandishi wa habari. Bwana Lucas Masungwa alisikika akiongea maneno yafuatayo wakati picha za tukio la gari kuungua pamoja na miili ya watu waliofariki dunia ikionyeshwa wazi;

*"...Hii ni breaking news kupitia hapa Global TV Online! taarifa zilizotufikia hivi punde ni kuwa watu wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 50 wanasadikika*

*kupoteza maisha kutokana na ajali ya gari aina ya lori linalobeba mafuta kuacha njia baada ya jitihada za dereva wa lori kutaka kumkwepa mtu aliyekuwa akivuka barabara eneo la Msamvu mkoani Morogoro..."*
*"...kwa mujibu wa mashuhuda, tukio hilo limetokea majira ya saa 3 asubuhi hii leo...tuendelee na jitihada za kumtafuta Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Morogoro ili kuthibitisha tukio hilo..."*

1.4 Global TV walirusha picha za watu waliofariki dunia katika ajali bila kuzingatia Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018 ambazo zinamtaka mmiliki wa mtandao azingatie weledi na maadili ya uandishi wa habari katika kuweka maudhui mtandaoni na kuhakikisha maudhui yake hayaleti usumbufu wa kisaikolojia kwa watazamaji wake au kusababisha woga/wasiwasi. Vile vile, kutoweka au kuonyesha kwa uwazi picha za majeruhi waliopata ajali au miili ya watu waliofariki dunia kwa ajali, au picha za watu waliouwawa.

1.5 Kitendo cha kuweka wazi na kurusha picha za miili ya watu waliofariki dunia, Global TV imekiuka Kanuni Na. 7 (1) (a) (b) na 12 (f), (h) (g)) za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mtandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo;

*7(1) A licence of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining and educating the public shall adhere to the following conditions:*
*(a) content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;*
*(b) adhere to journalism ethics and professionalism;*

*12. Online content services provider shall not publish-*
*(f) content that portrays violence, whether physical, verbal or psychological; that can upset, alarm and offend viewers and cause undue fear among the audience or encourage imitation;*
*(g) content that portrays sadistic practices and torture, explicit and excessive imageries of injury and aggression, and of blood or scenes of executions or of people clearly being killed;*

*(h) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder.*

## 2.0 WITO WA KUFIKA MBELE YA KAMATI YA MAUDHUI

Tarehe 23 Agosti, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Global TV,** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 28 Agosti, 2019, saa 08:00 mchana, uongozi wa Global TV ukiongozwa na Bw. Eric Shigongo James, Mmiliki wa Global TV na Mkurugenzi wa Global Publishers & General Enterprises Ltd aliyeambatana na Seleman E. Nyorobi, Mhariri Habari, na Abdallah Ng'anzi, Mkuu wa Global TV ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 3.0 KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI MTANDAONI YA GLOBAL TV

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Global TV** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 10 Agosti, 2019 yaliyochapishwa na Global TV katika chaneli yao mtandaoni ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 4.0 MAELEZO YA UTETEZI YA GLOBAL TV

Katika utetezi wao wa maandishi, Uongozi wa Global TV ulikiri kosa lao na kusema kuwa katika kuripoti tukio hilo, walichukua tahadhari kubwa ya kuziziba picha za miili ya watu waliokuwa wameungua katika ajali hiyo kwa kuwekewa kivuli lakini lilitokea tatizo la kiufundi na kuonesha picha hizo chini ya kivuli (transparent). Wameendelea kusema kuwa hawakuwa na nia ovu na kwamba hilo ni kosa lao la kwanza tangu walipopewa leseni. Wamemalizia kwa kuomba radhi na kuahidi kutorudia tena kosa na kusema kuwa maudhui hayo yasiyofaa walishayaondoa katika chaneli yao.

Pamoja na utetezi wao wa maandishi, Global TV waliendelea kueleza yafuatayo;

4.1 **Bw. Abdallah Ng'anzi** ambaye ni Mkuu wa Global TV alirudia utetezi wao kama walivyouandika katika maandishi.

4.2 **Bw. Eric Shigongo James** alianza kwa kukiri kosa lililofanyika. Alisema kuwa yeye binafsi hakuwa na taarifa ya kosa hilo mpaka alipotumiwa barua ya wito na Kamati kwa sababu kutokana na kazi nyingi alizonazo, huwa hayupo katika mnyororo wa wahusika wanaofanya uhariri wa kazi zao. Aliendelea kusema kuwa alipoiangalia video yao aliona kuwa aliyeiziba hakuwa makini na anatambua kuwa kwa upande wa mtazamaji ilikuwa inakera wakati kwa wafiwa au ndugu wa majeruhi ilikuwa inaumiza hisia. Aliomba radhi, na ikiwezekana wapatiwe nafasi nyingine na kuomba huruma ya Kamati katika adhabu kwa kusema kuwa hilo ni kosa lao la kwanza tangu kuanza kwa chaneli yao miaka saba iliyopita na kwamba hawatalirudia tena.

Alimalizia kwa kusema kuwa tangu wafanye kosa wamechukua hatua za kuiondoa video isiyofaa kwenye chaneli yao baada ya kupokea barua ya Kamati, wamemuandikia mwandishi aliyetenda kosa hilo barua ya onyo, na pia wamefanya mafunzo kwa wafanyakazi wao wote ili kuzidi kuwajengea uwezo katika masuala ya Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari. Alikabidhi barua ya onyo kwa Kamati na kuahidi kuwa kabla ya saa 12: 00 jioni ya tarehe 28 Agosti, 2019 watakuwa wameshatengeneza na kurusha video ya kuwaomba radhi watazamaji wao katika chaneli yao.

## 5.0 MAJUMUISHO YA UTETEZI WA GLOBAL ONLINE TV

Katika kujumuisha utetezi wao, **Bw. Eric Shigongo James** aliendelea kuomba radhi na kusema kuwa anautambua na kuuthamini sana mchango wa wajumbe wote wa Kamati ya Maudhui katika tasnia ya uandishi wa habari.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Global TV** imefanya kosa la kuchapisha maudhui yasiyofaa mtandaoni na kushindwa kuzingatia Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari.

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Global TV** kuwa waliziba picha zisizofaa kwa kivuli lakini likatokea tatizo la kiufundi hauna mashiko kwa sababu kitaaluma, inaonesha wazi kuwa mwandishi/mtaalamu wao wa picha alidhamiria kuziba picha kwa kivuli kinachoonesha kidogo (transparent) ili kuwatia shauku watazamaji wao kuangalia picha zisizofaa. Hata hivyo, Kamati (imetambua jitihada) walizozichukua Global TV kwa kuziba picha zisizofaa kwa kivuli kinachoonekana kidogo;

6.3 Kamati imebaini kuwa Global TV ina tatizo la usimamizi kwa sababu Mmiliki wake mwenyewe ameligundua kosa lao baada ya kupokea barua ya wito wa Kamati na pia video yao wameiondoa kwenye chaneli yao baada ya kupokea barua hiyo;

6.4 Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Global TV ya kuwafanyia wafanyakazi wake mafunzo ya kuwajengea uwezo katika Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari pamoja na kumpa barua ya onyo mwandishi aliyekosea baada ya kosa kutendeka;

6.5 Kamati imeridhishwa na ushirikiano walioonesha Global TV wa kukiri kosa lao, kuomba radhi, na kuahidi kutorudia tena;

## 7.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA GLOBAL TV

Kamati ina lengo la kuimarisha fani ya utangazaji na kamwe haina nia ya kubana au kuzuia ubunifu wa watangazaji, bali inawataka watangazaji kuboresha kazi zao kwa kuandaa na kutangaza maudhui yanayozingatia Weledi, Sheria, Kanuni na Maadili ya fani ya uandishi na utangazaji wa habari nchini.

Hata hivyo kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Global TV** yafuatayo: -

7.1 Kuimarisha usimamizi makini wa chaneli yao ili kuhakikisha kuwa maudhui yao ni salama kisheria kabla ya kuwekwa mtandaoni. Hatua hiyo itaiwezesha **Global TV** kuepuka kuvunja sheria na Kanuni za nchi.

7.2 Kuendelea kuwajengea wafanyakazi wao uwezo zaidi kupitia mafunzo ili waweze kuzingatia Sheria, Kanuni, weledi na maadili ya uandishi wa habari katika kazi zao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Global TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Global TV** kupitia chaneli yake mtandaoni imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kutoa adhabu zifuatazo kwa **Global TV**: -

1. **Wanapewa Onyo kali**;
2. **Kuomba radhi kwa Watanzania** kupitia Chanel yake kwa kosa lililofanyika kupitia chaneli yao iliyotumika kutendea kosa kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia tarehe 04 Septemba, 2019.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo ya tarehe **03** mwezi **Septemba** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeinengo-Sia Msoka**

..................................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ..........................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**.......................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**..........................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**...............................................